# HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI MHESHIMIWA DK. HUSSEIN ALI MWINYI KATIKA HAFLA YA KILELE CHA SHEREHE ZA MWEZI WA SHUKURANI NA FURAHA KWA WALIPA KODI KATIKA UKUMBI WA HOTELI YA GOLDEN TULIP ZANZIBAR

**TAREHE: 29 DISEMBA,2023**

**Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla;**
**Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid;**
**Spika wa Baraza la Wawakilishi,**

**Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdalla;**
**Jaji Mkuu wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Saada Mkuya Salum;**
**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango,**

**Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri Mliopo,**

**Mhandisi Zena Ahmed Said;**
**Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi,**

**Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya**
**Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wa Taasisi**
**mbali mbali za Serikali,**

**Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA),**

**Viongozi mbali mbali wa Vyama vya Siasa na Sekta binafsi**

**Walipakodi na Wageni waalikwa,**

**Waandishi wa Habari,**

**Ndugu Wananchi,**

**Mabibi na Mabwana**

**Assalamu Aleikum**

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa rehema kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana katika hafla hii ya siku ya kilele cha Sherehe za Mwezi wa shukurani kwa walipakodi ambayo huandaliwa maalum kwa madhumuni ya kutambua mchango wa walipa kodi wetu.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango na Mamlaka ya Mapato Zanzibar kwa maandalizi mazuri ya shughuli hii na kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi. Shukrani zangu za pekee nazitoa kwenu ndugu wafanyabiashara na walipakodi nyote kwa ushirikiano wenu na kwa kutimiza wajibu wenu wa kisheria wa kulipa kodi kwa hiari ili kuiwezesha Serikali kukusanya mapato ya kuendesha shughuli zake za kuwatumikia wananchi.

**Ndugu Wananchi na Walipa kodi,**

Nimepata faraja kujumuika pamoja nanyi katika sherehe inayoandaliwa kila mwaka na Mamlaka ya Mapato ya Zanzibar katika mwezi wa Disemba ambayo lengo lake kuu ni kujenga uhusiano mwema baina ya ZRA na walipa kodi, kusikiliza mahitaji yao, kuhamasisha ulipaji kodi wa hiari na kupokea maoni juu ya namna bora zaidi ya kuimarisha ulipaji kodi. Kwa msingi huo, hafla hii ina umuhimu wa kipekee kwa ZRA kupata wasaa wa kukaa pamoja na wateja wake ambao ni nyinyi walipa kodi kusikiliza maoni yenu ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Zanzibar kupata ufanisi katika kutimiza majukumu yake ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato Zanzibar.

Idadi kubwa ya washiriki wa shughuli hii na mafanikio ambayo nchi yetu inaendelea kuyapata katika kuongezeka kwa mapato yanayokusanywa na ZRA kila mwaka, yananipa faraja kuona kuwa mwamko wa ulipaji wa kodi kwa hiari hapa Zanzibar umazidi kuimarika.

Hali hii inanipa matumaini kwamba walipakodi mnajua wajibu wenu huo na kuamini kuwa hakuna nchi duniani ikiwemo Zanzibar inayoweza kupiga hatua za maendeleo bila ya kukusanya kodi zake kwa ufanisi. Mapato yanayotokana na kodi ni njia kuu na ya uhakika ya kuipatia fedha Serikali na kuiwezesha kutoa huduma ipasavyo kwa wananchi. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kukupongezeni walipakodi wetu kwa kulitambua hilo na kutimiza wajibu wenu. Hongereni sana

**Ndugu Wananchi na Walipa kodi**

Nimefurahi kusikia kuwa katika kipindi hiki cha mwezi mmoja, ZRA imekitumia katika kuimarisha matumizi ya mifumo ya kieleketroniki katika ukusanyaji wa mapato kwa kusimamia vyema mfumo wa utoaji wa risiti za kielektroniki (VFMS), na kutoa mafunzo yanayohusiana na jinsi ya kurekebisha risiti za kielektroniki zinazokosewa badala ya kuandika barua ZRA ili kuomba kufanyiwa marekebisho. Hii ni hatua nzuri na muhimu kwani inaondoa usumbufu na ina mchango muhimu katika kurahisisha ufanyaji wa biashara hapa Zanzibar.

Nawapongeza ZRA kwa jitihada zao za kuimarisha matumizi ya mifumo kwani nimeelezwa kuwa hivi sasa wanakamilisha utengenezaji wa mfumo mpya wa kusimamia ukusanyaji wa mapato ya kodi ZIDRAS unaoitwa (Zanzibar Integrated Domestic Revenue Administration System). Mfumo huu ambao nimeuzindua karibuni, umeanza kutumika mwezi wa Aprili, 2023 kwa kuwasajili walipakodi 2,340 wakiwemo walipa kodi wakubwa 186. Huu ndio mfumo utakaotumika badala ya mfumo wa ZITAS ulioanza kutumika tokea mwaka 2012 na kubainika kuwa na changamoto nyingi. Nimeelezwa kuwa mfumo huu wa ZIDRAS una manufaa mengi ambayo naamini mtapatiwa maelezo ya kina kuhusu faida zake. Napenda nikuahidini kuwa Serikali itaendelea kuwekeza katika mifumo ya uendeshaji

wa taasisi za kodi na shughuli zinazohusiana nazo kwa lengo la kurahisisha shughuli za biashara hapa nchini na kuweka usawa katika ukadiriaji na ulipaji wa kodi.

**Ndugu Wananchi na Walipa kodi,**

Ni jambo la kutia moyo kuona kuwa jitihada zetu za pamoja za kuimarisha ukusanyaji wa mapato kupitia ZRA, zinazidi kupata mafanikio. Kwa mfano tangu kuanza kwa mwaka huu wa fedha, katika kipindi cha miezi mitano, ZRA imepata mafanikio makubwa ambapo imeweza kuvuka lengo la makusanyo ya kodi yaliyowekwa kila mwezi na kuwa na ukuaji mzuri wa mapato ikilinganishwa na miezi kama hiyo mwaka jana.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 katika kipindi cha miezi mitano (5) yaani Julai hadi Novemba 2023, ZRA ilikadiriwa kukusanya jumla ya TZS bilioni 276.063. Makusanyo halisi ni TZS. Bilioni 288.251, sawa na ufanisi wa asilimia 104.42. Katika kipindi hiki cha Julai hadi Novemba 2023, ZRA imefanikiwa kuwa na ongezeko la ukusanyaji wa asilimia 21.93 ikilinganishwa na makusanyo ya TZS bilioni 236.407 ya kipindi kama hicho cha Julai hadi Novemba 2022. Kwa hakika haya ni mafanikio makubwa yanayoonesha mwelekeo mzuri katika ukusanyaji wa mapato ya kodi katika

mwaka huu wa fedha. Napenda niwashukuru sana viongozi na watumishi wote wa ZRA kwa mafanikio hayo. Pia nikushukuruni sana walipakodi kwa kuiwezesha ZRA kupata ufanisi huo.

**Ndugu Wananchi na Walipa kodi,**

Hali hii, inazidi kutupa imani kwamba kuna uwezekano wa kukusanya mapato zaidi na zaidi. Haya yatawezekana tu endapo changamoto zinazoelezwa na Walipakodi zitaondoka kwa kufanyiwa kazi na ZRA.

Nichukue fursa hii, kuwataka Wafanyakazi wa ZRA, kufanya kazi ya ukusanyaji wa mapato kwa Uadilifu na Uaminifu mkubwa. Kazi hii haifai kuambatana na vishawishi kutoka kwa Wafanyabiashara wachache wasiokuwa waadilifu. Serikali haitamvumilia Mfanyakazi yeyote wa ZRA na TRA Zanzibar, ambaye atakwenda kinyume na maadili ya Utumishi wa Umma wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Kwenda kinyume na maadili ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na wafanyabiashara katika kukwepesha mapato ya Serikali, ni kuidhoofisha Serikali katika kuwahudumia wananchi wake. Jambo hilo halivumiliki na wale ambao watabainika kufanya vitendo hivyo, hatua kali za kiutumishi na kijinai zitachukuliwa dhidi yao.

Kwa kuwa haki na wajibu ni watoto pacha, niwaahidi watumishi kuwa Serikali itaendelea kuyaangalia maslahi ya wafanyakazi wa ZRA kama vile ambavyo imekuwa ikifanya kwa wafanyakazi wengine wa Serikali ili kuongeza hamasa katika ukusanyaji wa mapato pamoja na kuiwezesha ZRA katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Aidha, niwaagize, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kuhakikisha wanakamilisha marekebisho stahiki ya mishahara ya watumishi wa ZRA, ili wapate faraja na waendelee na ufanisi katika kazi zao.

**Ndugu Wananchi na Walipa kodi,**

Lengo la Serikali ni kujenga utawala wa kodi utakaoiwezesha ZRA na Taasisi nyengine, kukusanya mapato yote ya Serikali yanayostahili, kwa urafiki zaidi na kurahisisha biashara Zanzibar. Nataka kuwahakikishia wafanyabiashara wote waliopo Zanzibar na wanaotaka kuja kuwekeza Zanzibar kwamba Serikali itaendelea kuimarisha mfumo wa kodi wa Zanzibar ulio rafiki na unaorahisisha biashara**.** Tutaendelea kuimarisha mfumo wa kodi ulio sawa kwa kila mfanyabiashara. Hakuna atakayependelewa wala kuonewa. Tutaendelea kuimarisha mfumo wa kodi ulio rahisi kuutumia (convenient) kwa kuwekeza zaidi katika mifumo ya kidigitali na kuwafikia walipakodi wengi zaidi kwa kuimarisha Ofisi za kodi

kila Mkoa na Wilaya za Zanzibar, tutaendelea kuimarisha mfumo wa kodi unao tabirika (certainty) kwa kuendelea kutoa elimu ya kodi ili kila mfanyabiashara ajue aina ya kodi anayostahiki kulipa na kwa wakati gani.

Natambua na kupongeza mageuzi na jitihada zinazofanywa na ZRA za kuanzisha na kuimarisha Ofisi za Mikoa kwa Unguja na Pemba kwa lengo la kurahisisha ulipaji kodi na kutatua changamoto za walipakodi waliopo katika Mikoa badala ya kutumia muda mrefu na gharama kufuata huduma hizo mijini kwenye Makao Makuu ya ZRA. Nazitaka Taasisi zote za Serikali zilizopo katika ngazi ya Mikoa na ngazi ya Wilaya zikiwemo Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa Ofisi hizi ili kuwezesha kufikia malengo. Aidha, Serikali itahakikisha kuwa ZRA inakuwa Taasisi ya kisasa ya ukusanyaji mapato katika ukanda wetu huu, Afrika na Duniani kwa ujumla. Hivyo, Serikali itatoa kila aina ya msaada kwa ZRA ili iweze kukusanya mapato zaidi kwa kadiri ukuaji wa uchumi wetu unavyoongezeka. Aidha, Serikali itahakikisha kwamba ZRA, inakuwa karibu na walipakodi kwa lengo la kutatua changamoto zao.

**Ndugu Wananchi na Walipa kodi,**

Naomba niwakumbushe wafanyabiashara wachache ambao wanafanya vitendo vya kupanga kupunguza bei za huduma na bidhaa kwa wateja wa nje ya Zanzibar ili mauzo na faida ibaki na kutozwa kodi nje ya Zanzibar (Transfer Pricing kwa baadhi ya Hoteli na Makampuni), kwamba vitendo hivi havikubaliki, na lazima ZRA na TRA Zanzibar wachukue hatua za kisheria kudhibiti uovu na uhalifu huu. Sote tunaelewa kwamba kulipakodi ni jambo la unapofanya biashara yoyote na popote pale duniani.

Aidha, nichukue fursa hii, kuwataka Maafisa Masuuli wote wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, ambazo zimepewa uwakala wa kuzuia kodi (Withholding Tax Agent) kutoka kwa wafanyabiashara wahakikishe kwamba wanazuia kodi hiyo, wanaiwasilisha ZRA na TRA Zanzibar kwa wakati kama sheria zinavyotoka hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali inawekeza pesa nyingi katika kujenga miundombinu Zanzibar. Serikali haitasita kumchukulia hatua Afisa Masuuli yoyote yule ambaye hazuwii kodi, au haiwasilishi kodi aliyozuwia kwa wakati na kwa ukamilifu.

**Ndugu Wananchi na Walipa kodi,**

Kabla ya kumaliza hotuba yangu, nawapongeza sana wafanyabiashara wote, wakubwa, wakati na wadogo wa Unguja na Pemba, ambao leo wamebahatika kushinda na watatunukiwa TUZO za ulipaji kodi vizuri Zanzibar, Hongereni sana. Nawashukuru sana kwa kutimiza wajibu wenu kwa Zanzibar.

Niwaombe hii iwe chachu kwenu kufanya vizuri zaidi kwa kulipa kodi kwa hiari mwaka ujao wa 2024. Pia niwatie moyo wale ambao hawakubahatika kushinda TUZO mwaka huu wasikate tamaa. Hii iwahamasishe kufanya vizuri zaidi kwa mwaka 2024 ili muweze kushinda TUZO za mwakani. Naomba mjuwe kuwa Serikali inawatambua na kuwathamini sana.

Nataka pia nitowe wito kwa wananchi wa Zanzibar kuziunga mkono ZRA na TRA Zanzibar, katika jitihada zao za ukusanyaji wa mapato ili mapato hayo yaweze kutumika katika kuiwezesha Serikali, kutoa huduma zote muhimu kwa wananchi kwa kiwango cha hali ya juu. Mengi yanayofanywa na Serikali hii yanaweza kufanyika kutokana na ukusanyaji mzuri wa mapato unaofanywa na taasisi hizi.

Aidha, nitumie fursa hii kuwataka wananchi wote wakubwa na wadogo kudai risiti kila wanapofanya manunuzi, kwani kwa kufanya hivyo ndipo watakapoiwezesha ZRA kukusanya kodi yote ambayo wananchi hao wanailipa wakati wanapofanya ununuzi wa biadhaa na huduma kutoka kwa wafanyabiashara.

**Ndugu Wananchi na Walipa kodi,**

Namalizia kwa kukushukuru wewe binafsi Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar, uongozi na wafanyakazi wa ZRA kwa jitihada ambazo mmekuwa mkizichukuwa katika kuhakikisha kwamba mapato yanakusanywa kwa ufanisi.

Aidha, nimshukuru Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi na Wajumbe wake kwa usimamizi mzuri wa taasisi hii na kuweza kufikia mafanikio haya. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa usimamizi mzuri wa ukusanyaji kodi na kwa kunipa fursa hii ya kuwa Mgeni Rasmi Katika hafla hii ya kilele cha Mwezi wa Shukrani na Furaha kwa walipakodi hapa Zanzibar kwa mwaka 2023. Tumuombe Mwenyezi Mungu aizidishie nchi yetu amani, umoja na mshikamano. Mwenyezi Mungu atuwezeshe kuitekeleze mipango yetu ya maendeleo kwa mafanikio zaidi. Nakutakieni nyote kila la kheri.

**“Tulipe Kodi kwa Maendeleo ya Zanzibar”**

**Asanteni kwa kunisikiliza.**